TANGAZO LA SERIKALI NA. 528 la tarehe 28/6/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# AMRI

(*Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

AMRI YA KUTANGAZA MABADILIKO YA MPAKA WA MSITU WA HIFADHI TAMBURU YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Mabadiliko ya Mpaka wa Msitu wa Hifadhi Tamburu ya Mwaka 2024.

Tangazo

Ts. Na. 132 la 1930

2. Eneo la ardhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Tangazo la Msitu wa Hifadhi Tamburu linafanyiwa mabadiliko kusomeka na kuonekana kama lilivyochorwa katika Ramani iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA RUFIJI


MSITU WA HIFADHI TAMBURU

Makadirio ya Eneo: Hekta 5251.84 au Kilometa za Mraba 52.52

Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la ardhi awali chini ya Msitu wa Hifadhi Tamburu linalopatikana Wilaya ya Rufiji, Mkoa wa Pwani kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 2884 ya mwaka 2014 (Skeli 1:20,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:

*Tangazo la Serikali Na. 528 (Linaendelea)*




Dodoma,
24 Mei, 2024

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*